


Redio ya Desimali

desimali




Age
Umri
7+




Siku moja Ngedere alikuwa anaendesha gari lake. Ghafla gari likazima.




Oooh! Mafuta yameisha.




Rafiki yake, dereva wa bodaboda, akampa lifti
ili aende kituo cha mafuta kununua mafuta.




Njiani wakawa wanasikiliza kipindi cha redio kilichotoa ushauri wa biashara. “Kama unataka unaweza kusikiliza tena, ni FM 102 na nusu,” dereva wa bodaboda alisema.




Wakafika kituo cha mafuta.



Ngedere akanunua mafuta.




Akarudi kwenye gari lake na kujaza mafuta.




Akawasha gari.



Akawasha redio na kujaribu kutafuta 102 na nusu.



Lakini hakupata hiyo stesheni.



Bahati nzuri Kibena na Kiduchu walitokea walikuwa njiani kwenda kucheza mpira.



Ngedere akawaomba wamsaidie
kumfungulia redio 102 na nusu FM kisha
atawapeleka uwanjani kucheza.



Kiduchu akamwambia

102 na nusu FM


ni sawa na

102 nukta tano FM.

$$102\frac{1}{2} = 102.5$$



Akanyoshea kidole sehemu ya 0.5 na kusema,
“Stesheni ipo hapa!”




Ngedere hakuelewa. “Mbona hamna sehemu palipoandikwa nusu?” Kibena akamwambia, “Ngoja nikuelezee vizuri.




Unakumbuka ulipojifunza sehemu na namba?”
“Ndiyo nakumbuka, chungwa langu lilikatwa katika
vipande vinne,” alijibu Ngedere.



“Uliniambia kuwa naweza kukata chungwa langu katika vipande vinne na kila kipande nikauza kwa shilingi hamsini.”



“Sawa, ila leo nitakufundisha njia nyingine
ya kuonyesha sehemu. Hii inaitwa **desimali**.”



Katika **DESIMALI**, namba yoyote kabla
ya desimali ni **namba nzima**...

1.234




na namba yoyote baada ya desimali
ni ndogo kuliko namba nzima.


1.234




Kwa hiyo, stesheni imeandikwa 102 na nusu FM
ndiyo unayoita futa na inaweza pia ikaandikwa
102 nukta tano FM.”




Ngedere hakuelewa bado.




Kibena akaonyesha alama ndogo ambazo ziko kati ya 102 na 103 na kusema,
“Kati ya 102 na 103 kuna sehemu kumi tofauti.




Katika sehemu kila kijisehemu ni sawa na moja ya kumi, mbili ya kumi, tatu ya kumi na kadhalika.



Katika desimali kila kijisehemu ni sawa na **sifuri nukta moja**, **sifuri nukta mbili**, **sifuri nukta tatu** na kadhalika.



Kwa hiyo **tano ya kumi** ni sawa na **sifuri nukta tano**.



Angalia **sifuri nukta tano.**

Namba ya kwanza baada ya desimali
inaitwa **makumi.**



Kwa hiyo **sifuri nukta tano** katika desimali ni sawa na **tano ya kumi** katika sehemu.

$$0.\textcolor{red}{5} = \frac{\textcolor{green}{5}}{\textcolor{green}{10}}$$




Tano haigawanyiki kwa kumi. Kwa hiyo tunaandika **sifuri na kuweka alama ya desimali**. Kumi inaingia mara ngapi katika hamsini? **Ni mara tano**. Kwa hiyo jibu ni sifuri nukta tano.


$$10 \overline{) 5} = \overline{) 5.5}$$




Unaweza kuona hapa, tano ya kumi au nukta tano ni kati ya 102 na 103.




Kwa hiyo hii ndiyo stesheni uliyokuwa unaitafuta.
Dereva wa bodaboda alikuchanganya kwa kuiita 102 na
nusu FM. Ndiyo maana hukuweza kuipata. Ilibidi aseme
102 nukta 5!”




“Kibena, kama Ngedere hajaelewa hiyo, hataelewa tena.
Twende tukacheze mpira,” alisema Kiduchu.



“Nimeelewa sasa! Naelewa
DESIMALI!” Ngedere alisema kwa furaha.



Akawaambia wapande gari na atawapeleka
kuwachukua Koba na Baraka.



Koba na Baraka walifurahi kuona Kibena
na Kiduchu wamekuja na gari. Lakini Koba alisema,
“Haibadilishi mchezo. Sisi wanaume tutashinda tu!”





Mwisho

Imeandaliwa na

ubongo.co

Haki zote zimehifadhiwa.
Hairuhusiwi kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa njia
ya aina yoyote bila idhini ya mwandishi,
UBONGO INTERNATIONAL.